

HABARI KASKAZINI



Taasisi za umma zaagizwa kujeungu eGA

Na Cynthia Mwirolezi,
ARUSHA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene ameziagiza taasisi za umma kujeungu mifumo bora ya Serikali Mtandao (eGA) ili kuharakisha utoaji huduma kwa wananchi.

Waziri Simbachawene alitoa agizo hilo jana jijini hapa wakati akifungua kikao kazi cha nne cha eGA.

Vilevile, aliagiza taasisi zilizopo chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kutupiwa jicho la karibu kwa kuwa nyangi zilizoko pembezoni mwa nchi hazijajunga na mifumo huo.

"Taasisi za umma kujeungu na mifumo huu ni lazima na siyo hiyari ili kuharakisha utoaji wa

huduma kwa haraka wananchi.

"Hapa napenda kupongeza Idara ya Mahakama imepiga hatua kubwa katika eneo hilo. Lakini zipo taasisi za umma zinaingia katika mifumo kwa kulega lega hawa wanaita kwa sababu zao, sasa ni lazima taasisi zote ku-harakisha zinajungu na mifumo huu," alisema. Kuhusu serikali za mitaa, alisema serikali inapoteza mapato mengi kutokana na kutoqua na mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ukiwemo wa Tausi, mahususi kwa kufanya malipo pamoja na kuchelewesha kutoa huduma kwa wananchi. "Fedha nyingi za serikalini zinakaa kwenye mikono ya watu kwa muda mrefu bila sababu na hii inatokana na baadhi ya taasisi za umma, zikiwemo hamashauri kutotumia mifumo wa TEHAMA na kuhuishwa kwa wakati," alisema.

Simbachawene, alisema seri-

kali inapenda kuona kila taasisi ya umma inaweka mkakati wa kuharakisha mifumo yote ya mtandao inabadilisha taarifa zake na ili kufanikisha hilo, ni lazima zijiunge.

Vilevile aliagiza kuanzia kikao kazi cha mwaka ujao, wana-toa tuzo kwa washindi wa mifumo huo wa TEHAMA ili kuleta ushindani zaidi katika utendaji kazi.

Kwa mujibu wa waziri huyo, Katibu Mkuu, Juma Mkoni, Tanzania ni mionganini mwa nchi ukanda wa jangwa la Sahara inaongoza kwa matumizi ya eGA.

Katibu Mkuu, Juma Mkoni, alisema kikao hicho kimehudhuriwa na wadau kutoka mashirika na taasisi za umma, wakiwemo maofisa masuuli, wakurugenzi na wakuu wa vitengo vya TEHAMA na watumiaji wengine wa mifumo ya teknolojia hiyo.

"Mwaka jana tulifanya kikao

- kazi cha tatu cha Serikali Mtandao na kuweka maazimio 12, katika kikao hiki tutawasilisha taarifa ya utekelezaji wa maazimio hayo ni wakati mzuri kwa washiriki kufahamu yale waliyokubaliana na kutekeleza," alisema

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Selestine Kakele, alisema wizara yake inasimamia jukumu la kutunza ulinzi na usalama wa wananchi na kutoa huduma bora kwa jamii bila ubaguzi kwa kutumia TEHAMA.

Makamu Mwenyekiti wa Bodii ya eGA, Dk. Jasmine Kusekwa, alizitaka taasisi za umma kutekeleza maagizo ya matumizi ya TEHAMA kwa kuwa ni takwa la kisheria.

Kaulimbiu ya kikao hicho kwa mwaka huu ni 'Kuharakisha uz-ingatiwaji wa sera, sheria viwango na miongozo ya serikali mtandao, kwa ubadilishaji salama wa taarifa'.